

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **MAPENDEKEZO YA BEI YA KUNUNULIA UMEME TOKA KWA WAZALISHAJI WADOGO WADOGO KWA MWAKA 2011**

Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini na kwa msaada wa Benki ya Dunia inapenda kuharakisha huduma ya umeme iwafikie watazania wengi zaidi. katika utekelezaji wa mradi wa Nishati Tanzania (TEDAP), Serikali inaendeleza miradi ya umeme itokanayo na nishati jadidifu (renewable energy) hapa nchini kwa kuwavutia wawekezaji binafsi ili washiriki katika kuanzisha miradi midogo midogo ya umeme.

Ili kufanikisha lengo hili, Wizara ya Nishati na Madini, kwa kuwahusisha wadau mbalimbali, ilitayarisha mfumo rahisi wa utekelezaji wa miradi midogo midogo ya umeme isiyozidi megawati 10, unohusisha (1) Mkataba wa Ununuzi wa Umeme (*Standardised Power Purchase Agreement*) na (2) Mfumo wa Kukokotoa Bei ya Kununua Umeme (*Standardised Power Purchase Tariff*) zitakazotumika kuunganisha na kuuza umeme katika Gridi ya Taifa na Gridi ndogo (*isolated mini-grid*). Mfumo huo uliidhinishwa na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa mujibu wa kifungu namba 17 cha Sheria, Sura ya 414 (EWURA Act, Cap 414).

Utaratibu wa kukokotoa bei ya umeme unaweza kufanyiwa marekebisho kila baada ya miaka mitano, isipokuwa kama kuna jambo la msingi linalotakiwa kurekebishwa. Bei ya umeme kwa miradi midogo midogo inarekebishwa kila mwaka kulingana na mabadiliko ya gharama za uendeshaji zilizo nje ya uwezo wa mwekezaji. Bei hiyo hurekebishwa na Kikosi Kazi cha Maendeleo ya Miradi Midogo Midogo (*Working Group on Small Power Development (WGSPD)*) ambacho kinawezeshwa na EWURA.

Wawakilishi wa WGSPD wanatoka Wizara ya Nishati na Madini, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baraza la Ushauri la Watumiaji Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (CCC), "Tanzania Private Sector Foundation", Wakala wa Nishati Vijijini (REA), TANESCO huku EWURA akiwa kama mtazamaji (observer). Wawakilishi hao hukutana kila mwisho wa mwaka, na kwa kutumia taarifa zilizowasilishwa na TANESCO, hukokotoa bei ya umeme kwa miradi midogo midogo kwa mwaka ufuatao. Kikosi Kazi hicho sasa kimekamilisha na kuwasilisha EWURA kwa kuidhinishwa mapendekezo ya bei kwa mwaka 2011 kama inavyooneshwa hapa chini:

- (a) Bei iliyopendekezwa kwa mwaka 2011 ya kununulia umeme toka kwa Wazalishaji Umeme Wadogo wadogo waliounganishwa katika Gridi ya Taifa imeoneshwa katika Jedwali Na. 1:

**Jedwali Na. 1: Bei ya Umeme kwa Wazalishaji wadogo wadogo – Gridi ya Taifa**

Wastani wa bei ya Umeme kwa Wazalishaji Wadogo wadogo			112.43	TZS/kWh
Bei itabadilika kulingana na msimu	Msimu wa jua/kiangazi	Agosti - Novemba	134.92	TZS/kWh
	Msimu wa mvua/masika	Januari - Julai na Desemba	101.19	TZS/kWh

- (b) Bei iliyopendekezwa kwa mwaka 2011 ya kununulia umeme toka kwa wazalishaji umeme wadogo wadogo waliounganishwa katika Gridi ndogo ndogo (Isolated grid) imeoneshwa katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2: Bei ya Umeme kwa Wazalishaji Wadogo wadogo – Gridi ndogo**

Wastani wa bei ya Umeme kwa Wazalishaji Wadogo wadogo	380.22	TZS/kWh
-------------------------------------------------------	--------	---------

Kwa mujibu wa kifungu namba 19 (2) (b) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 (EWURA Act, Cap 414), wadau wote wanakaribishwa kuwasilisha maoni yao, kwa barua au vinginenvyo, juu ya uhalali wa Bei ya Ununuzi wa Umeme toka kwa wazalishaji umeme wadogo wadogo katika kipindi cha wiki tatu (siku 21) tokea tarehe ya tangazo hili.

Maelezo zaidi yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya EWURA, [www.ewura.go.tz](http://www.ewura.go.tz) au kwa kuandika barua kwa:

**Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)  
S.L.P. 72175,  
Dar es Salaam  
Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)**

Limetolewa na:  
**Mkurugenzi Mkuu,  
EWURA  
18 Februari 2011**